

MAELEZO YA MSINGI KUHUSU NYANYA -Tomato(*Lycopersicon esculentum*)

Nyanya ni zao ambalo hulimwa kwa kiasi kikubwa katika maeneo mengi duniani kote. Asili yake ni kutoka Amerika ya kusini na kati. Nyanya ni miongoni mwa mazao jamii ya mboga mboga ambazo hulimwa na wakulima wengi. Tunda la nyanya hutumika kama kiungo muhimu katika mapishi na utengenezaji wa kachumbari. Nyanya ni chanzo kizuri cha vitamini mwilini na hutengeneza kipato kizuri kwa mkulima kama zikilimwa vizuri kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo na uzalishaji. Zikiwa kama kiongeza ladha muhimu kwenye chakula, nyanya huhitajika zikiwa mbichi au zikiwa zimesindikwa kutengeneza bidhaa nyinginezo kama vile nyanya za kopo na tomato sauce.

Kwa muda mrefu sasa uzalishaji wa zao la nyanya umekuwa chini ya kiwango katika sehemu nyingi za Tanzania na hii inatokana na matumizi ya mbegu zisizokuwa na kiwango, kanuni duni za uzalishaji wa mazao, ukosefu wa zana za kilimo, idadi kubwa ya wadudu waharibifu na magonjwa.

HALI YA HEWA, UDONGO NA MAJI

Kwa kawaida nyanya huhitaji hali ya hewa iliyotulia na kavu ili kuweza kufanya vizuri. Lakini nyanya humudu mazingira mengi. Mazingira yenye baridi kali au joto kali huharibu ukuaji pamoja na uzaaji wa nyanya. Udongo wowote wenye virutubisho hai unafaa kupandia nyanya kinachotakiwa ni kuhakikisha kuwa udongo unaweza kuupa mmea chakula kiasi kinachohitajika kukua na kuzaa. Matumizi ya maji yanatakiwa yaangiliwe vizuri ili kuhakikisha kuwa maji hayazidi wala kupungua kwani maji mengi husababisha mizizi kuoza, ni chanzo cha magonjwa na mmea kudumaa.



1. NAMNA YA UZALISHAJI WA MBEGU ZA NYANYA

Ili kuweza kuzalisha mbegu binafsi za nyanya inatakiwa kutumia aina za nyanya za kawaida na siyo chotara (Hybrid F1). Kwani chotara haziwezi kupandwa zaidi ya mara moja (mzunguko mmoja wa upandaji).

Kanuni za kufuata katika uzalishaji wa mbegu za nyanya

- ✓ Mbegu ya nyanya inatakiwa izidishwe mara moja tu na siyo zaidi
- ✓ Eneo lenye nyanya za mbegu liwe mita 25 kutoka kwenye nyanya zisizokuwa za mbegu
- ✓ Kusiwe kumewahi kupandwa nyanya hivi karibuni katika eneo la uzalishaji
- ✓ Mmea wa nyanya uchunguzwe kwaajili ya wadudu na magonjwa
- ✓ Matunda ya mwanzo yasitumike katika utolewaji wa mbegu
- ✓ Baada ya mbegu kuota, vijimeme vingine ving'olewe mapema
- ✓ Kuondoa magugu, kulimia na matunzo mengineyo yaendele

Utaratibu wa kutoa mbegu

- Chagua matunda yaliyokomaa na kuiva vizuri kutoka katika fundo au tawi la pili la nyanya. Hakikisha nyanya hazina dalili ya ugonjwa wala kushambuliwa na wadudu wa aina yoyote.
- Safisha nyanya vizuri ili kuondoa uwezekano wa kushambuliwa na ugonjwa.



i) Kukamua mbegu kutoka kwenye nyanya

ii) Mbegu kavu zilizohifadhiwa

- Kata nyanya kwa kuigawanya katikati kisha tumia kijiko au kamua kwa kutumia mkono kutoa mbegu kuweka kwenye bakuli.
- Funika bakuli kwa kutumia kitambaa au karatasi ili kuzuia uchafu usiingie lakini usiifunike kabisa kiasi cha kukosa hewa.
- Ziache mbegu zikae kwa kati ya siku 1 hadi 5 (2 hadi 3 kwa maeneo yenye joto). Zikoroge kila siku ili zichachuke kwa pamoja na kuzuia ubadilikaji wa rangi.
- Tumia maji masafi kuosha mbegu. Kama kuna mbegu zinazoelea wakati wa kuosha zitolewe kwani zitakuwa hazijakomaa au kujaa vizuri.
- Kausha mbegu kwenye eneo ambalo lina hewa ya kutosha na mwanga usiokuwa wa moja kwa moja.
- Kama mbegu hazipandwi wakati huu, zinatakiwa zihifadhiwe kwenye mfuko au chombo ambacho kinaweza kuzuia maji kuingia ndani. Inashauriwa kuweka majivu chini ya chombo cha kuhifadhiwa mbegu ili kuzuia uwezekano wa unyevu nyevu kujijenga na zichunguze mara kwa mara kuhakikisha ziko salama.
- Mbegu zilizokaushwa na kuhifadhiwa vizuri huweza kukaa kwa miaka miwili bila kuharibika. Kilo moja ya nyanya kuweza kuzalisha kati ya gramu moja hadi nne za mbegu.

Aina ya mbegu za nyanya

Kawaida	Chotara (Hybrid F1)
CAL - J	Bingwa F1
Moneymaker (Duara)	Kartik F1
Tanya	Asilia

Kumbuka kuwa mbegu za chotara (hybrid F1) hutumika mara moja tu na hivyo hazifai kutengeneza mbegu.